

MKATABA WA UPANGAJI

MKATABA huu umetayarishwa leo tarehe 04 mwezi 12.mwaka 2023

KATI YA

RAHIDI MOHAMED wa Dar es salaam Tanzania (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama “**MWENYE NYUMBA**”) kwa upande mmoja.

PERFECT TEXTILE INDUSTRY LIMITED wa Dar es salaam (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama “**MPANGAJI**” kwa upande mwingine.

NA KWA VILE Mwenye NYUMBA amekubali kupangisha na Mpangaji amekubali kupangishwa sehemu ya nyumba (Chumba) hiyo iliyopo **ILALA CBD** Mtaa wa **KARIAKOO**, kata ya **KARIAKOO**, Barabara **SIKUKUU**, Namba ya nyumba **56**, Block **003**.

HIVYO BASI Makubaliano hayo yameshuhudia yafuatayo:-

1. MUDA WA MKATABA

Mkataba huu utakuwa wa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia tarehe 04 Mwezi 12 mwaka 2023 na utamalizika tarehe 03 mwezi 12 mwaka 2026

2. KODI

Mwenye nyumba amekubali kupangisha na mpangaji amekubali kupangishwa katika sehemu hiyo ya nyumba kwa madhumuni ya kufanya biashara kwa kulipa kodi ya shilingi milioni moja na nusu (1,500,000) kwa mwezi mmoja. Wakati wa kutiliana saina mwenye nyumba amekubali kupokea Tsh milioni arobaini na tano (45,000,000) Ikiwa ni malipo ya miaka mitatu.

3. NI WAJIBU WA MPANGAJI KUTEKELEZA YAFUATAYO:-

- (a) Kutopangisha Mtu mwingine katika nyumba hiyo bila idhini ya Maandishi ya Mwenye nyumba
- (b) Kulipia gharama zote za umeme katika chumba hicho kwa kipindi cha Mkataba.
- (c) Kuweka chumba na mazingira yake katika hali ya usafi na kufanya matengenezo madogo madogo inapobidi na gharama za matengenezo kwa matumizi yake hazitakuwa jukumu la Mwenye nyumba
- (d) Iwapo makubaliano hayo hayataongezwa muda wake, atamkabidhi Mwenye nyumba sehemu hiyo ikiwa tupu.

4. NI WAJIBU MWENYE NYUMBA KUTEKELEZA YAFUATAYO:-

- (a) Kuweka nyumba katika hali nzuri
- (b) Kutombughudhi Mpangaji wa chumba hicho anayesimamia kwa masharti yaliyopo.

5. INAKUBALIWA PIA KUWA

- (a) Endapo Mpangaji atakuwa na Nia ya kuendeleza atawajibika kutoa taarifa ya Maandishi ya mwezi mmoja kabla ya kipindi cha Mkataba kuisha.
- (b) Kama Mpangaji hatakabidhi nyumba hiyo kama walivyokubaliana basi Mwenye nyumba ana haki ya kumtoa kwa kutumia Dalali yeyote bila amri yoyote ya Mahakama.
- (c) Mgogoro wowote utatokea kuhusiana na Mkataba huu, basi mgogoro huo utatambuliwa kufuatana na sheria za nchi.

Mkataba huu umeshuhudiwa na wahusika kwa kutia sahihi zao katika namna na katika tarehe, mwezi na mwaka unaoonekana hapa chini.

UMESAINIWA na KUTOLEWA na RAHIDI MOHAMED ambaye amekubaliwa Na ambaye namfahamu hapa Dar es salaam Leo 04 mwezi 12 mwaka 2023.

}
MWENYE NYUMBA

UMESAINIWA na KUTOLEWA Na PERFECT TEXTILE INDUSTRY LIMITED ambaye amekubaliwa Na ambaye namfahamu hapa Dar es salaam Leo 04 mwezi 12 mwaka 2023.

}
MPANGAJI

SHAHIDI;

JINA **DANIEL SIMON**
SAHIHI
ANWANI **105069 DSM**
KAZI **WAKILI**

